Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, toeni katika vitu vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyowatoleeni katika ardhi, wala msikusudie (kutoa) vilivyo vibaya, ambavyo ninyi wenyewe msingevipokea isipokuwa macho yenu yakiwa yameinamishwa chini kwa huzuni na aibu, na jueni kwamba Allah ni Mkwasi, Asifiwaye. (2:268)

JUZU 80 No. 216 | DH.QAD-DH.HIJ.1440AH | JULAI 2020 | WAFA 1399 HS | BEI TSH. 500/=

Kuitafuta Haki kwa Njia Sahihi



Makala uk 1

Habari za Ghaib Zadhihirisha Ukweli wa Ahmadiyya

Na Sheikh Bakri Abedi Kaluta

Ukweli wa Ahmadiyya wathibitika kutokana na baadhi ya matukio yake kuwa yalishabashiriwa tangu zama za kale na watakatifu wa Mungu waliopashwa habari hizo makhsus za Ghaib, ambazo zimehifadhiwa ndani ya ushahidi wa maandiko na historia.

Kama nilivyoandika hapo awali kuhusiana na bishara alizozisema Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as], za matukio yatakayokuja kutokea katika zama za Khalifa wake wa nne, ambapo, Masheikh wenye misimamo mikali, wataanzisha fitna kubwa dhidi ya Jumuiya, lakini msaada wa Mwenyezi Mungu utakuwa pamoja na Jumuiya yake.

Ndani ya Kitabu cha Hadithi za Mtume Muhammad[saw]. cha Jaamii Tirmidhi, Kitabus swaum, Bab maa jaa a fii swaumil Muharrami, kuna Hadithi iliyosimuliwa na Khalifa wa nne wa Mtume Muhammad[saw], Hadhrat Ali[ra], Hadithi ambayo ilikuja kutimia katika zama za ukhalifa wa nne wa Mtumishi wa Mtume Muhammad[saw], Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as], Imam Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa[as] Hadithi hiyo yasema kwamba Mtume Muhammad[saw] alisema kwamba:

"*Ikiwa mwahitaji kufunga swaumu katika mwezi mwingine wowote ule minghairi ya mwezi wa Ramadhani, basi fungeni swaumu katika mwezi wa Muharram, kwa sababu ndani ya mwezi huo, Mwenyezi Mungu Aliwaokoa wana wa Israeli dhidi ya Firauni kutokana na Toba yao. Na vivi hivi, katika zama zijazo pia, za watu wa mwishoni, Mwenyezi Mungu Atalirudia tukio kama hili.*" Firauni na watu wake waligharikishwa na Allah mnamo siku ya JUMATANO ndani ya mwezi wa MUHARRAM. (Durrun Manthur, Jal. 6 cha Imam Suyutwi). Hizi ni bishara za tangu enzi za Mtume wetu Muhammad[saw] zilizolenga kututayarishia mazingira watu wa zama zetu hizi, za kumtambua mja mkubwa wa Allah aliyekuwa adhihiri katika zama hizi za Aakhiruz Zamaan, yaani zama za Mwisho. Mwenyezi Mungu Akatoa uthibitisho kwa mja huyo, Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa, Mirza Ghulam Ahmad[as], pale alipomfunulia Wahyi zenye kutoa fafanuzi za yale yaliyobashiriwa na Mtume Muhammad[saw].

Mnamo usiku wa tarehe 21 December 1902 kuamkia tarehe 22 December 1902, ndani ya usiku wa kwanza wa kumi za mwisho za Ramadhani, Hadhrat Ahmad[as] alipokea ufunuo kutoka kwa Allah usemao: "*Ya atii 'alaika zamanun ka mithli zamani Musa, yaani zitakufikia zama kama zama zilizomfikia Musaas*" (Al Hakam jal. 6 No. 46 la tarehe 24 December 1902 uk. 11-14 na Al Badar Jal.1 No. 9 la tarehe 26 December 1902 uk. 71, Hali kadhalika ndani ya uk. wa 446 wa Tadhkira).

Endelea uk. 5

Muongozo kwa Waqifeen-e-Nau uk. 5

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Nuru ya Kiroho na Kimwili

Tatizo kubwa la watu wa magharibi ni ulimbukeni unaotokana na maradhi ya kujigamba kuwa kila kitu kizuri, maendeleo tunayoyaona katika Nyanja zote yametoka kwao. Kabla ya wao lilikuwa giza tupu. Hakuna chembe ya ukweli katika fikra hizo. Wanahistoria wamefanya kazi ya kuthibitisha kuwa nuru inayomulika duniani hivi leo inachomoza kutoka jangwa la Uarabuni iliyoletwa na Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w).

Kwa mfano katika upotofu wao watu wa magharibi wanaamini kuwa dhana ya haki za binaadamu imetoka kwao hususani katika katiba yao, na makubaliano yao yanayoitwa Magna Carta ya Uingereza. La kushangaza ni kuwa Magna Carta imekuja karne sita baada ya Islam. Yote hayo yaliyosimamiwa na Magna Carta yalikuwa kwenye karatasi. Miaka mingi baadae ndio ikazaliwa tangazo la uhuru na katiba ya Marekani. 1789 palitokea mapinduzi huko Ufaransa yaliyodai kusimama kwenye haki, usawa na utu. Si katiba ya Marekani au mapinduzi ya Ufaransa viliyoleta haki za binadamu. Watu wengi nchini Marekani waliendelea kunyonywa na kunyanyaswa. Mfano wa hivi karibuni ni wa George Floyd alivyoteswa hadi kufariki. Ufaranssa iliwapokonya watu wa Afrika Maghalibi utamaduni na uhuru hadi wakashika mtutu wa bunduki ili kujikomboa.

Haki za binadamu katika Islam hazitokani na mapenzi ya mtawala au kufurahi kwake. Haki za binadamu katika Islam zimetoka kwa Allah, hazikutoka kwa bunge, mfalme, au kiongozi. Si zawadi au hisani kutoka kwa mtu yeyote isipokuwa ni hidaya kutoka kwa Aliyetuumba hivyo hakuna anayeweza kuibadilisha na kuivunja haki hiyo. Na kwa njia yeyote ile anayepokonywa haki hiyo lazima aliyepokonya airudishe haki hiyo ima fa ima. Ndio maana katiba hizi zilizotengenezwa na binadamu ni dhaifu na hazikidhi mahitaji. Katiba ya kuongoza binadamu na kupata ustawi ilitekelezwa kwa vitendo mjini Madina na Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. Ingawaje tumesema kuna ulimbukeni wa kufikiri maendeleo yote tunayoona yametoka magharibi tumepata katika tenga letu la historia la samaki walioza mmoja ambaye yuko salama.

Peter Frankopan ni Profesa wa historia katika Chuo Kikuu cha Oxford ambaye ameandika kitabu chake maarufu *The Silk Road: A New History of the World*, ambacho kinakubaliwa kuwa ni kitabu bora duniani kwa historia ya dunia. Msomi huyu ameonyesha kuwa mwanzilishi wa utamaduni wa mapatano ya watu wa makabila tofauti, rangi tofauti, kuheshimu dini za watu wengine, alikuwa ni Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. Katika mji wa Madina haki ilitendeka kwa wote, haki ya kuabudu iliheshimiwa. Huu ni mfano unaong'aa wa kuonyesha kuwa tatizo la ubaguzi wa rangi, kudharau na kubeza dini za wengine na viongozi wao ni maradhi yanayoweza kufutika katika jamii. Na yalifutika mjini Madina na popote palipoota mizizi ya Islam.

Profesa Frankopan anaendelea kueleza kuwa wakati Ulaya imo katika giza totoro, wasomi bora duniani walikuwa wamekusanyika katika miji ya Bukhara, Merv, Gurdrshapur, Ghazm kwa ajili ya kukuza elimu na utafiti. Wakati ulimwengu wa Kiislam unaenzi utafiti, Mtakatifu Augustine alisema watu wanapenda kujua kwa ajili tu ya kupenda kujua ingawaje elimu haina faida kwao. Kupenda kujua ni maradhi. Hiyo ndiyo Ulaya inayojitapa hivi leo. Lakini mapenzi ya utafiti ndiyo yameupatia ulimwengu Abu Rayhan Al Birun ambaye aliwafungua macho watu wa Ulaya kuwa dunia ndiyo inayozunguka jua, Abu Ali Hussayn Ibn Sina, bingwa wa hesabu, Ibn Al Haytham aliyebuni miwani kwa kuwataja wachache.

Tuna jukumu sisi Waislam kuelewa historia na mchango wetu katika maendeleo. Mwendo huo unaweza kutokomeza utamaduni wa vijana wetu kuhusudu kila takataka inayotupwa kwetu. Tunayo maji safi yaliyotoka mbinguni kwa nini tupapatikie maji yaliyotuama ambayo tukinywa tunapata maradhi?

Kuitafuta Haki kwa Njia Sahihi

Imefasiriwa na
Ahmad Abdul Nasibu

Hakuna mwanadamu asiye na hatia angepaswa kufa namna George Floyd. Yalikuwa ni mauaji ya kinyama.

Lakini kifo cha George ni tukio pekee, ambalo kwalo afisa wa usalama akawa jambazi na kuvunja kiapo cha maadili alichoapa kukilinda? Au George ni ukatili wa hivi karibuni katika mnyororo mrefu wa mauaji ya kikatili?

"***Uliniahidi hutoniua!***" Natasha McKenna (Februari 2015)

"***Nashindwa kupumua!***" – Freddy Gray (Aprili 2015)

*"**Sitaki kufa ningali mdogo!**"* – Christian Taylor (Agosti 2015)

*"**Nashindwa kupumua!**"* – Eric Garner (Julai 2014)

*"**Sina bunduki. Wacheni kupiga risasi!**"* – Michael Brown (Agosti 2014)

*"**Tafadhalini msiniache nakufa!**"* – Kimani Gray (Machi 2013)

*"**Kwa nini umenipiga risasi?!**"* – Kendrec McDade (Machi 2012)

*"**Mnanifuatilia kwa lipi?**"* – Trayvon Martin (Februari 2012)

*"**Maafisa, kwa nini mmechomoa bunduki zenu?!**"* – Kenneth Chamberlain (Novemba2011)

*"**Umenipiga risasi! Umenipiga risasi!**"* – Oscar Grant (Januari 2009)

Wanaadamu hawa, kama mahala pengine pale, wangekuwa hai leo endapo rangi za ngozi zao zingekuwa nyeupe, kama wasingefanya "makosa" ya kuwa weusi katika nchi inayowabeua.

Na baadhi ya Waamerika wamechoshwa. Wananchi wanaingia mitaani kugomea Serikali ambayo kiasili imezoroteshwa na mfumo baguzi wa rangi, ambayo inachana taswira safi ya jamii yetu kwa kuua watu watu wasio hatia kwa jina la haki.

Halafu, tumekwama katika mduara wa makosa, ambapo ubaguzi wa kimfumo husababisha migomo. Hii migomo halafu inatekwa na wezi wadogo wadogo na kuongezeka hadi kuwa fujona uporaji, ambayo inadumisha zaidi ubaguzi wa kimfumo dhidi ya Waamerika Weusi. Tunalazimika kuvunja mduara huu, licha ya tamaa ya asili ya kupaisha hasira zetu mitaani, licha ya kisasi tunachokitamia kinagaubaga. Khalifa wetu ametuelekeza kufanya hivyo. Kuhusu kuandamana, Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba}, amefundisha:

"***[Mara nyingi], waandamanaji hupora au kuharibu mali na vitu aidha vilivyo miliki ya taifa au wananchi binafsi … Hata ambapo maandamano au migomo inafanyika kwa amani, bila ya kupelekea kwenye uharibifu wa kihalifu au fujo, bado inaweza kuwa na madhara hasi sana.***

"***Hii ni kwa sababu hata migomo ya amani mara nyingi huleta hasara ya mamilioni kwenye uchumi wa taifa. Si katika hali yeyote iwayo tabia namna hiyo inaweza kufikiriwa kama mfano wa uaminifu kwa taifa.***" (Hotuba katika Makao Makuu ya Jeshi. Koblenz, Ujerumani, 20 Mei 2012)

Hatuwezi kuzichoma nyumba zetu katika upingaji ili kuwafanya wazisikie sauti zetu. Tutabakia na mkaa na majivu tu. Khalifa wetu ametuelekeza kuzitoa hasira zetu na kuadabisha katika namna tofauti kabisa. Tunalazimika kufanya sauti zetu zisikike, sio mitaani kupitia migomo,


George Floyd

bali kwenye sanduku la kura. Tunapaswa kuzitumia haki zetu za kupiga kura na kuwaondoa wale viongozi waliochaguliwa ambao wanaziunga mkono sera ambazo zinachochea chuki. Haki yetu ya kupiga kura ndiyo itakayoifanya Serikali ambayo inaunga mkono mfumo baguzi wa rangi kuteketelea chini.

Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba}, anathibitisha hili, akisema:

"Iwapo mtu au kundi linataka kuibadili Serikali, basi wafanye hivyo kwa kufuata mchakato unaostahili wa kidemokrasia"

"Wanapaswa wafanye wasikike kwa kupiga kura kwenye sanduku la kura … Hii ndio Islam ya kweli."

(Mtu mwingine vile vile)

Mwanaharakati, Michael Render aliwahutubia waandamanaji na kuwashauri:

"***Sasa, ni muda wa kupanga, kunuia, kuweka mkakati, kuratibu na kuhamasisha. Ni muda wa kuwang'oa waendesha mashtaka msiowapenda katika kibanda cha kura. Ni muda wa kuziwajibisha ofisi za ma-Meya, Machifu, na Manaibu wao.***" (CNN, Killer Mike anawasihi waandamanaji wa Atlanta '***kutochoma nyumba zao***' katika ombi la hisia)

Novemba 3 ipo karibuni. Katika miezi mitatu tu, Uchaguzi wa Marekani 2020 utafanyika. Nafasi zote 435 katika Bunge la Marekani, nafasi 35 kati ya 100 katika Seneti ya Marekani na ofisi ya Rais wa Marekani zitagombaniwa.

Hakuna kiasi chochote cha migomo, uporaji au fujo za mitaani zitakazomrudisha hai George Floyd. Lakini kuitumia haki yetu ya kupiga kura na kuzibadili sura za viongozi kunaweza kutuhakikishia kwamba maisha ya asiyehusika mwingine hayataporwa mikononi mwetu.

Msiruhusu George Floyd afe bure. Piga kura!

Wacha pia tukumbuke maneno haya ya Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba}:

"Ni wajibu wa wanachama wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kuziombea pande zote mbili kuacha matendo mabaya ya kupindukia na ukatili. Wale wanaoweza kusaidia kutengeneza mazingira ya amani ndani ya duru zao za ushawishi waweke bidii kufanya hivyo. Allah Mwenye Nguvu Aiokoe dunia kutokana na hali ya kutotawalika na Ajaalie machafuko na migongano haraka igeuke katika hali ya amani." (Hotuba ya Ijumaa, 9 Januari 2015)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Muongozo kwa Wazazi wa Waqifiin-e-Nau

Ahmad Abdul Nasibu



Khalifa Mtukufu wa V^atba akihutubia Ijtimaa ya mwaka ya Waqf-e-Nau (Atfal na Khuddam) Uingereza 7 Aprili 2019

Ilikuwa ni wakati wa mwanamke mtawa, mama wa Mariam na mwanamke wa Imran ambapo alisema *'Mola wangu, hakika nimeweka nadhiri Kwako aliyomo tumboni mwangu kuwa wakfu; basi nikubalie. Bila shaka Wewe ndiwe Usikiaye, Ujuaye.*

Mnamo 3 Aprili 1987, Hadhrat Khalifatul Massih IV^rh alipendekeza kwa Jumuiya kufuata sunna za Mitume na kutoa ile miliki yao azizi-, mwana wao atarajiwaye kuzaliwa katika njia Allah, katika kusudi la Islam, utapanyaji wa Ahmadiyya na huduma kwa ubinadamu. Kumtoa mtoto wako kwa Allah ni tukio lililo kubwa mno na si kitu cha kawaida na ni aina ya zawadi ambayo mtu anapaswa kuiwasilisha kwa Allah katika namna iliyo nzuri. Uzuri wa binadamu ni kupitia Taqwa yake - utawa. Kwa hiyo, kabla hawa watoto hawajakua kufikia umri ambao wanatakiwa 'kukabidhiwa' kwa Jamaat, wazazi wao wana wajibu mzito mno.

Katika hotuba yake ya Ijumaa, huzur^rh alisema: *"Allah Ameielekeza nadhari yangu katika suala hili ili kwamba niwaombeni muweke nadhiri kwamba watoto watakaozaliwa kwenu katika miaka miwili ijayo, iwe wa kiume au kike, watolewe katika Waqf kama zawadi kwa Allah. Wakina mama waja wazito ambao hawakuweza kushiriki katika katika mpango huu hapo kabla wanaweza kushiriki sasa. Pia wanaweza kuweka nadhiri. Lakini nadhiri hii inatakiwa kuwekwa na wazazi wote wawili. Wanatakiwa kuamua katika hili kwa pamoja, ili kwamba kuwe na umoja wa kimalengo katika ukuzaji na elimu ya watoto hawa. Na wanapaswa kuanza kuwafunza katika namna iliyo bora tangu utotoni mwao."*

Mwanzoni mpango ulianzishwa kwa miaka miwili, lakini ukaongezwa hadi minne na baada ya hapo ulifanywa wa kudumu kwa sharti jipya kwamba wale wazazi wanaotamani kuyatoa maisha ya watoto wao lazima wafanye hivyo kabla ya kuzaliwa.

Mnamo tarehe 10 na 17 Februari 1989, Huzur^rh alitaja baadhi ya majukumu ya wazazi kwa Waqifeen-e-Nau ambayo nitayaaorodhesha baadhi hapa chini:

1. Wazazi wanapaswa kuchunga watoto wao kwa ukaribu.
2. Watoe umakini maalum katika masuala muhimu ya malezi ya tabia.
3. Endapo wazazi wanafikiri mtoto wao hastahili kwa Waqf, basi wamwogope Mungu na kuitaarifu Jamaat.
4. Wazazi wanapaswa kufunza upendo na ukweli katika nyoyo za watoto wao.
5. Wazazi watalazimika kushughulikia malezi yao kabla ya kuwafundisha watoto wao.
6. Wazazi wanapaswa kuwa waangalifu na makini wakati wa mazungumzo majumbani mwao na kujiepusha na kila ya aina ya utetaji.
7. Wanapaswa kufundishwa kuridhika na kuchukia uroho wa mali na kujipatia vitu.
8. Wazazi wanapaswa kuwasaidia watoto wao kujipatia viwango vya juu vya uaminifu na ukweli.
9. Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao kuwa wacheshi na uchangamfu.
10. Uchangamfu na uvumilivu ni viwango viwili ambavyo Waqifeen-e-Nau wanapaswa kufundishwa.
11. Tokea mwanzoni, Waqifeen-e-Nau wanapaswa kufundishwa Qur'an Tukufu.
12. Wazazi wanapaswa kuisanikisha kwa mtoto wao tabia ya kuisoma Qur'an Tukufu kila siku na kwa utambuzi.
13. Wazazi wanapaswa kuhakikisha kwamba watoto wao wana elimu kubwa ya dini na kisekula.
14. Wazazi wanapaswa kujiunga kwenye magazeti na majarida kwa ajili ya watoto wao.
15. Wazazi wanapaswa kuiingiza kwao taratibu tabia ya kusoma vitabu ambavyo vitawaongezea elimu.
16. Pindi Waqifeen-e-Nau wanapoenda shule, wazazi wanapaswa kuwachagulia masomo ambayo kwao yatawaleta kwenye sayansi. Wanapaswa kuwa na elimu ya masomo yote anuwai.
17. Waqifeen-e-Nau wanapaswa kufunzwa uvumilivu na stahamala.

Hivyo, nataka kufikisha kwa wakina mama na baba hao kwamba jina tu la Waqf-e-Nau halitoshi. Kwa usahihi, Waqf-e-Nau ni wajibu muhimu. Ni wajibu wa wazazi hadi Waqf-e-Nau anapokuwa mtu mzima na baada ya hapo inakuwa ni wajibu wake.

18. Waqifeen-e-Nau wanapaswa kufundishwa tokea utotoni tabia ya kusema kile kinachofahamika kuwa ukweli kama kweli na kilicho dhana kuwa dhana.
19. Wanapaswa kufundishwa kupiga chapa.
20. Wanapaswa kufundishwa namna ya kutunza hesabu. Kuwepo na msisitizo mkubwa juu ya uaminifu.
21. Huzur^atba amesema *"Mataifa makubwa hujengwa majumbani mwao"*
22. Tokea utotoni, Waqifeen-e-Nau wanapaswa kufanywa imara na watiifu kwa Nizaam-e-Jamaat.
23. Wazazi hawapaswi kusema lolote dhidi ya Nizaam-e-Jamaat majumbani mwao.
24. Waqifeen-e-Nau wanapaswa kuandaliwa kuwa viongozi wakubwa.
25. Fundisha utiifu kwa watoto wenu.
26. Elezea kwa watoto wenu kwamba Waqf ni suala zito; kwamba ni kiapo ambacho umekula na Allah.
27. Huzur^rh alisema *"Hapo mwanzo nilipata nafasi ya kutembelea Disneyland huko Marekani. Kulikuwa na bembea ambayo ilikuwa na kona za hatari mno na kasi ya ajabu. Ilikata kona za ghafla ambazo zinaweza kuwa hatari kwa watu wenye udhaifu wa moyo. Kwa hiyo waliweka mabango ya tahadhari yakisema kwamba unaweza kurudi nyuma katika hatua hii na mwishoni kulikuwa na onyo katika wekundu lililosema; **"Huu ndio mwisho. Sasa huwezi kurudi nyuma."** Kwa hiyo, kutakuwa na 'lango' ambapo watoto ambao wametolewa masiha kwa Waqf sasa, wataambiwa, "Huu ni mlango wa mwisho baada ya huu huwezi kurudi nyuma. Kama una ujasiri wa kuuza maisha yako, kama unaweza kutoa kila kitu kwa Allah bila kigeugeu, ndipo tu uje mbele waila rejea mara moja." Kwa hiyo watayararisheni kupita lango hili sasa."*
28. Ni muhimu na inajuzu kutilia maanani kwenye afya yao ya kimwili tangu utotoni. Wanapaswa kutiwa moyo kushiriki katika michezo.
29. Wawekeni mbali na vitabu/ maandiko ya kipuuzi.
30. Msisitizo mkubwa unapaswa kuwekwa katika Kiarabu na Kiurdu. Baada ya hizo lugha zao za asil. Kichina na Kirusi pia ni muhimu.
31. Maadili yao mazuri yapaswa kuzikonga nyoyo za watu.
32. Waqifat-e-Nau wanapaswa kufundishwa menejeimenti ya nyumbani na hesabu za nyumbani.
33. Waqifat-e-Nau wafundishwe ufundishaji, udaktari, sayansi ya kompyuta, upigaji taipu, lugha.
34. Msisitizo mkubwa uwekwe kwenye sala ili wawe na mahusiano ya karibu na binafsi na Allah tangu utotoni.

Hizi zilikuwa nukta ambazo Hadhrat Khalifatul Masih IV^rh alizitaja katika hotuba zake za Ijumaa. Wazazi wazisikilize hotuba kamili mbazo pia zinapatikana katika sehemu ya 'Rasilimali' [Katika tovuti ya waqfenauintl. org].

Endelea uk. 4

Muongozo kwa Wazazi wa Waqifiin-e-Nau

Kutoka uk. 3

Wazazi wana wajibu mkubwa kwa kuwa watoto wao wa Waqf-e-Nau watakuwa viongozi wa baadaye wa taifa. Tarbiyyat ina mchango mkubwa, na mfano wa kwanza watoto wauonao ni ule wa wazazi wao. Kwa ajili ya hilo wazazi pia wanaombwa kufanya yafuatayo:

1. Faili binafsi linapswa kuundwa kwa kila mtoto wa Waqf-e-Nau. Faili hili linatakiwa lijumuishe cheti cha kuzaliwa, barua ya kukubaliwa Waqf-e-Nau, rekodi za chanjo, n.k. Maendeleo ya mtoto wako yanatakiwa pia kuhifadhiwa katika faili hili, k.m. tarehe ambayo Yassarnal Quran ilimalizwa, tarehe ambayo Salat ilikaririwa, na ripoti za shule kutoka shuleni. Nakala ya faili linatakiwa kutunzwa na katibu wa mahali pale wa Waqf-e-Nau. Mnapohamia kwenye mji mwingine, faili hili linatakiwa kupatiwa katibu mpya wa Waqf-e-Nau. Nakala za nyaraka zote zitumwe Makao Makuu ya Taifa ili rekodi kuu ziendane na muda na kamilifu.

2. Wazazi wanapaswa kutumia tabia ya wastani katika malezi ya mtoto. Mtoto asitendewe ama kwa ukali uliopitiliza wala kwa upole kupitiliza.

3. Malezi ya mtoto yapaswa kufanywa kwa mfano binafsi. Wazazi wanatakiwa kuziendeleza tabia zote zile kwao wenyewe ambazo wangependa kuziona kwa watoto wao.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih V[atba] ametoa hotuba nyingi na hotuba za Ijumaa kuhusiana na majukumu ya Waqifeen-e-Nau na wazazi wao. Akiwahutubia wazazi, Huzur[atba] ametaja katika hotuba yake mnamo 06 Mei 2012 katika msikiti wa Baitul Futuh *"Ningependa pia kuwanasihi wazazi wa Waqf-e-Nau kuhusu malezi ya watoto wao. Wanatakiwa kusimamia na kutoa malezi ya kimaadili ya watoto wao wote na sio tu kwa wale walio sheemu ya mpango wa Waqf-e-Nau… Unatakiwa ukumbuke daima kwamba iwapo mwanaoa mkubwa ni Waqf-e-Nau, kisha ukashughulikia malezi yake ya maadili sawasawa, atakuwa mfano chanya wa kuigwa kwa nduguze wadogo. Kwa namna hii, watajifunza kutokea kwenye tabia yake nzuri."*

Kisha,mpendwa wetu Huzur[atba] alisema katika hotuba yake ya kihistoria ya Ijumaa mnamo 28 Oktoba 2016 *"Malezi ya kila mtoto wa Kiahmadiyya yanategemeana na wazazi na wazazi wanataka mazuri kwa watoto wao. Wazazi ambao wameielekea dini, wanataka elimu yake ya sekula, malezi na elimu ya dini pia. Lakini likumbukwe hili kwamba, kila mtoto, hususan mtoto wa Waqf-e-Nau ni amana ya Jamaat waliyo pamoja nayo. Malezi yake na kumfanya kuwa sehemu bora ya Jamaat na jamii, ni wajibu wa wazazi. Lakini, malezi ya watoto wa Waqf-e-Nau, elimu yao ya sekula na dini kwa uangalizi maalum, inakuwa wajibu kwa sababu nyingineyo pia. Ya kwamba, kabla ya kuzaliwa, wazazi wanaahidi chochote kitakachozaliwa, kike au kiume, watakitoa kwa ajili ya dini ya Allah, kwa ukamilishaji wa jukumu la mtumishi wa kweli wa Mtukufu Mtume (amani iwe juu yake) ambalo ni jukumu la kumalizia uzagazaji wa muongozo, ambalo ni jukumu la kueneza elimu ya Islam duniani, ambalo ni jukumu la kuvuta nadhari ya dunia kwenye kutimiza haki za Mungu ambalo ni jukumu la kuzagaza elimu ya Islam ya kutimiza haki za pande mbili za kila mtu duniani.*

Tena Huzur[atba] akasema katika hotuba hiyo hiyo ya Ijumaa *"Hivyo kile wazazi watakachokitia kidogo kidogo akilini mwa watoto wao tangu mwanzo kwamba wao ni watoto wa Waqf-e-Nau na wao [wazazi] wamewatoa kabisa kuhudumu imani. Na hili ni lengo la maisha yao [watoto], nao watakuwa wakiomba pia, ndipo watoto watakuwa na akili kwamba wanatakiwa kuihudumu imani. Hawatakuwa wakifikiria kuwa wafanya biashara au wachezaji, au kwenda kwenye kada fulani. Badala yake, watauliza swali kwamba wao ni Waqifeen-e-Nau na Jamaat au Khalifa wawaambie kada ipi waingie. Hawana mnasaba na dunia."*

Huzur[atba] pia alitaja katika hotuba hiyo hiyo ya Ijumaa kwamba wazazi wanapaswa kuwa mfano kwa watoto wao na kwamba maneno yao na vitendo virandane. Huzur[atba] alisema *"Nataka kuwaambia wazazi kwamba haijalishi ni malezi kiasi gani wanayatoa kwa mdomo, hayatakuwa na athari mpaka maneno yao na vitendo hayapishani. Wazazi wanabidi kuziboresha hali zao za sala. Wanatakiwa kujenga mipangilio ya kusoma na kuifundisha Qur'an Tukufu. Watatakiwa pia kuwa mfano wa kuigwa wa maadili ya juu. Wao wenyewe watatakiwa kuelekea utafutaji wa elimu ya dini. Viwa ngo vya juu vya kuchukia uwongo vinapaswa kupatikana. Licha ya madhara yafanywayo na baadhi ya wahudumu wa ofisi, wanatakiwa kujiepusha na kuongea majumbani mwao, dhidi ya mfumo wa Jamaat au wahudumu wa ofisi zake. Katika MTA, walau hotuba zangu zitatakiwa kusikilizwa bila kukosa."*

Ningependa kumaliza sehemu hii kwa nukuu ya mpendwa wetu Huzur[atba], ambamo amesema *"Hivyo, nataka kufikisha kwa wakina mama na baba hao kwamba jina tu la Waqf-e-Nau halitoshi. Kwa usahihi, Waqf-e-Nau ni wajibu muhimu. Ni wajibu wa wazazi hadi Waqf-e-Nau anapokuwa mtu mzima na baada ya hapo inakuwa ni wajibu wake."*

Allah Atuwezeshe kutimiza wajibu huu mkubwa katika kila namna bora inavyowezekana. Amin

Maarifa Juu ya Jahanamu na Peponi

Na **Musa Salum Mgeleka**
Dar es Salaam

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ تُوبُوٓاْ إِلَى ٱللَّهِ تَوۡبَةٗ نَّصُوحًا عَسَىٰ رَبُّكُمۡ أَن يُكَفِّرَ عَنكُمۡ سَيِّـَٔاتِكُمۡ وَيُدۡخِلَكُمۡ جَنَّٰتٖ تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ يَوۡمَ لَا يُخۡزِي ٱللَّهُ ٱلنَّبِيَّ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مَعَهُۥۖ نُورُهُمۡ يَسۡعَىٰ بَيۡنَ أَيۡدِيهِمۡ وَبِأَيۡمَٰنِهِمۡ يَقُولُونَ رَبَّنَآ أَتۡمِمۡ لَنَا نُورَنَا وَٱغۡفِرۡ لَنَآۖ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ قَدِيرٞ

[Surat At-Tahrim 9]

Enyi mlioamini! Tubuni kwa Allah toba iliyotakasika; huenda Mola wenu Akawafutieni maovu yenu na kuwaingizeni katika Pepo zipitazo mito chini yao, siku ambayo Allah Hatamfedhehesha Mtume na wale walioamini pamoja naye; nuru yao itapiga mbio mbele yao na upande wa mikono yao ya kuume; watasema: Mola wetu, Ututimizie nuru yetu, na Utughofirie; hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

MAARIFA YA KWANZA - MENDELEO YASIO KOMA

Mwanadamu ameumbwa kwa kupewa Maendeleo yasiyo kuwa na Kikomo na kama vile Mimea. Aya hii 66:9 inaeleza jambo hili kuwa maendeleo ya mwanadamu hayana mwisho. Hata watu wa Peponi watahitaji hatua moja zaidi ya nyingine.

Mwanadamu amelinganishwa na Mimea. Quran Tukufu imesema mwanadamu amepatikana kama vile Mimea wanavyoota. Surah 71:18 Na Mwenyezi Mungu Akawaotesheni katika ardhi kama mimea:

Maendeleo ya Mimea yapo kwenye Kifo na Uhai. Yaani Mahindi mfano yanapooteshwa hukuwa na kukomaa kisha hukauka/ Kufa na Uhai wake hubaki katika punje za mbegu. Na zikipandwa huota tena na kuwa Mahindi yale yale na sio Mtama. Na ndivyo Binadamu naye Ametokana na Kifo na Uhai;

Surah 2:29
Mtamkataaje Mwenyezi Mungu na hali mlikuwa wafu naye Akawahuisheni, kisha Atawafisheni, kisha Atawahuisheni, kisha Kwake mtarejeshwa?

Kuwa mwanadamu alikuwa Mfu akahuishwa, kisha Atakufa na kuhuishwa tena. Kifo chetu sio mwisho wetu. Kama ilivyo mbegu ya mahindi hutiwa ardhini ili kuota ndivyo mwili na Roho huwekwa kaburini ili kuota kama Mmea vile/ kupatikana mwili mwingine.

Surah 80:18-23
18. Aangamizwe mtu! Mbona anakufuru sana! 19. Kwa kitu gani Amemwumba? 20. Kwa tone la shahawa; Amemwu-mba na Akamwezesha. 21. Kisha akamfanyia njia nyepesi, 22. KISHA AKAMFISHA na AKAMWEKA KABURINI, 23. KISHA APENDAPO ATAMFUFUA.

Kanuni hii ya maendeleo ndio kanuni ya jumla ya Ulimwengu wote. Kwa Kuumba Hasara na Faida, Shida, Dhiki, Njaa, Mahitaji na Haja n.k kumevifanyi vitu vyote kuendelea daima pasipo ukomo. Juhudi za Mwanadamu nazo hazina mwisho wake, hii ni Ishara tu kuwa Uhai huu baada ya Kifo hauna Ukomo, waila mtu atazaliwa Upya katika Umbo la KIROHO.

Maendeleo ya mwanadamu pia Daima huendelea kuwa na Mawasiliano hata na Wafu. Roho za watu baada ya Kufa huendelea kuwepo na mara kadhaa hufanya Mawasiliano na wapendwa wao kwa njia mbalimbali kama vile NJOZI na KASHFI. Hata dini za Jadi huwa na dhana hii ya kuendelea kufanya mawasiliano na Wafu kwa jina la MIZIMU. Dhana hii ys Mizimu iwe ya kweli au sio kweli ila wana nadharia ya kweli juu ya uwepo wa mawasiliano ya wafu na watu wazima. Nadharia hii isingekuwepo ikiwa mtu baada ya kifo ndio mwisho wake. Kuna mifumo mbalimbali ya watu waliozitengeneza ya mawasiliano kama vile Simu. Simu moja ikifa na nyingine ikabaki nzima, ileyo nzima hainauwezo kwa namna yeyote kufanya mawasiliano na iliyokufa. Wala ushahidi huu haupatikani katika viumbe wengine zaidi ya mwanadamu. Ni mwanadamu tu ndio ana NJOZI na KASHFI na ndio huweza kufanya mawasiliano na hata Roho za viumbe wengine (wakiwa hai viumbe wengine huweza pia kufanya mawasiliano ila sio wakifa)

Maendeleo mengine ya viumbe kuwa kila kitu chenye Umbo baada ya Kifo chake hutengeneza Umbo lingine.
Surah 17:50-52
50. Na wakasema: Je, tutakapokuwa mifupa na chembe zilizosagika, je, tutafufuliwa kuwa viumbe wapya? 51. Sema: Kuweni mawe au chuma, 52. Au kiumbe katika vile vinavyoonekana vigumu katika mioyo yenu (hata hivyo mtafufuliwa). Hapo watasema: Ni nani atakayeturudisha? Sema: Ambaye Aliwaumbeni mara ya kwanza. Ndipo watakutikisia vichwa vyao na watasema: Yatakuwa lini hayo? Sema: Huenda yakawa karibu.

Sayansi imehakiki juu ya rasilimali kama madini, Gesi, ardhi, viumbe wengine n.k hutokana na Vifo vya Viumbe. Wadudu mfano huzalika kwenye mwili uliooza/ Uchafu n.k.

Kama Mwili baada ya Kifo hujipatika Mwili mpya ndivyo kwa Roho nayo itajitengenezea mwili wake wa Kiroho. Maendeleo haya ya Kiroho huendelea mpaka kufikia zama za Ufufuo.

Maisha ya Ufufuo yanalinganishwa na maisha mengi ila kwa leo mfano utatolewa kwa kulingana na Mfumo wa Uzazi. Mama anapobeba ujauzito, kichanga huendelea taratibu hatua kwa hatua mpaka muda unapofika uchungu humkamata mama na Kuzaliwa Dunia. Duniani anakumbana na dunia ya matendo, Raha na Shida. Ndipo baada ya maendeleo baada ya kifo wanadamu wote watafufuliwa au watazaliwa ili kupatiwa ladha zao za Pepo na Jahanamu. Huu utaitwa ni ufufuo wa mara ya pili baada ya ule wa tumbo la Uzazi.

Katika matoleo yajayo tutaangalia Maarifa ya Pili na ya tatu juu ya Jahanamu na Peponi Insha Allah
Mola wetu, tumiminie uvumilivu na Utufishe watii/ Waislamu. Amin

Habari za Ghaib Zadhihirisha Ukweli wa Ahmadiyya

Kutoka uk. 1



Na wahyi ule wa mwaka 1882 niliouandika mwanzoni kabisa ulifafanua kuwa, zama hizo zitakuwa ni zama za Khalifa wake wa nne, kwa jinsi alivyojiona kuwa amekuwa Hadhrat Ali*ra* aliyekuwa Khalifa wa nne wa Mtume Muhammad*saw*., na Hadhrat Ali ndiye mtu ambaye aliisimulia Hadithi hiyo ya bishara ya tukio kama la Muharram litakalotokea katika zama zetu hizi za mwisho. Si vibaya nikiinukuu tena Ruya hiyo ya Hadhrat Ahmad*as* iliyosema Hivi:

'Nilijiona kuwa nimekuwa Hadhrat Ali Karramal Laahu wajhahu. Na katika hali hiyo kulikuwa na tukio fulani ambapo kulikuwa na kundi fulani la makhawaarij (waasi) waliokuwa wakiupinga Ukhalifa wangu, yaani kundi hilo lilikuwa likitaka kulizuia Jambo la Ukhalifa wangu na kuingiza fitna ndani yake. Hapo nikamuona Mtume Muhammad*saw*. akiwa pamoja nami, akiniambia kwa huba na upendo, akisema: Ewe Ali, achana nao hao na wasaidizi wao na shamba lao, waepuke. Na nikakuta Kwamba, katika wakati huo wa fitna, Mtume saw akiniasa na kunisisitiza nifanye subira akiniambia: 'Wewe ndiwe uliye juu ya haki, lakini ni bora uache kuongea na watu hao.' Na shamba mradi wake ni kundi lile la watu walio wafuasi wa Masheikh, walioathirika na mafundisho yale waliokuwa wakipatiwa tangu kitambo Fulani na Masheikh wao hao. Kisha hali yangu ikaelekea tena kwenye Ilhaam na kwa njia ya Ilhaam, Mwenyezi Mungu Akanidhihirishia mtu fulani anayenipinga akisema kunihusu mimi kwamba: Dharuunii Aqtulu Musa, yaani niacheni nimuue Musa, yaani mimi. Na ndoto hii niliiona mnamo takriban usiku wa saa tisa kasoro dakika ishirini hivi na asubuhi yake ilikuwa ni siku ya JUMATANO.' (SIKU ALIYOGHARIKISHWA FIRAUNI NA MAJESHI YAKE).

Halafu mnamo tarehe 18 march 1907, Hadhrat Ahmad*as* alipata ufunuo mwingine uliosema: "Kuna Musa fulani Nitakayemdhihirisha Nami Nitampa heshima mbele ya watu." (Tadhkira uk. 706).

Funuo hizo za fafanuzi za bishara hizo, hazikuishia tu kwa Hadhrat Ahmad*as*, bali hata Khalifa wake wa pili, Hadhrat Mirza Bashirud Din Mahmud Ahmad*ra* (Aliyetajwa kwenye ufunuo wa Muslih Maud kuwa na roho ya Kimasihi), pia aliendelezewa silsila hiyo ya kupokea funuo za ufafanuzi wa bishara hizi za zama zetu hizi za mwisho. Akitoa maelezo ya aya ya 11 ya Sura Al Fajr isemayo: Wa Firauna dhil awtaad na Firauni mwenye majeshi, Hadhrat Muslih Maud*ra* anasema:

"Baada yake (aya ya 10) Akamtaja Firauni. Kwa rai yangu hii ni habari ya zama za Masihi Aliyeahidiwa*as* Hadi sasa siwezi kueleza kwa kina ni kwa nini, lakini kuna mambo mawili ambayo ninayaeleza, ambayo kimsingi yaweza kusemwa kwamba, mfano huu wahusiana na zama za Masihi Aliyeahidiwa*as* na mambo hayo mawili ni haya: Kwanza Mtume Mkarimu*saw*. anasema: 'Usiku wa tarehe 10 wa Muharram una shani na taadhima makhsus kwa sababu katika siku hiyo Mungu Alimuokoa Musa dhidi ya Firauni nami natumai kwamba katika siku zijazo hali ya aina hii hii itatokea tena katika umati wangu ambapo umati wangu utaokolewa na adhabu fulani katika siku hiyo.'

Ingawa kwa dhahiri hapa kuna maneno ya kuokolewa dhidi ya Firauni na dhulma zake, lakini ishara hii yapatikana humo kwamba, tukio la aina hii litatokea katika siku zijazo.

Dalili ya pili ni hii kwamba Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa anasema: Nilijiona nikiwa nimesimama kwenye mto Nile nikiwa na wana wa Israeli wengi sana, nami nikiwa najifahamu kuwa ndiye Musa*as* Yaonekana tulikuwa tumekimbia. Nilipotazama nyuma nikafahamu kuwa Firauni alikuwa akitufuatilia akiwa na jeshi kubwa sana pamoja na vifaa vingi sana kama vile farasi, magari ya farasi ya kubebea silaha na ya kupigania vita n.k. nao wakawa wametukaribia sana. Wana wa Israeli waliokuwa nami wakahofu mno na wengi wao wakawa wamekata tamaa na wakaanza kupiga kelele kwa sauti ya juu wakisema ewe Musa, tumekamatwa. Hapo nikasema kwa sauti ya juu; Kallaa, inna ma'iya Rabbii sayahdiini, yaani kamwe hakika Mola Wangu yu pamoja nami, Ataniongoza. Hapo nikaamka wakati ulimi wangu ukiendelea kuyatamka maneno haya. (Tadhkira uk 429).

Halikadhalika kuna Wahyi wake mwingine alioupokea usemao: 'Ya'atii 'alayka zamanun ka mithli zamani Musa (Tadhkira 423). Yaani itakujia zama itakayokuwa kama zama ya Musa. Hivyo, wakati ndani ya Hadithi kuna ishara hii kwamba tukio fulani lifananalo na lile lililotukia katika zama za Musa*as* litatokea katika umati wake, na historia yashuhudia kuwa hadi sasa halijawahi kutokea tukio la aina hiyo, upande mwingine amekuja yule aliyetumwa na Mwenyezi Mungu katika zama hizi, naye akiambiwa kuwa yeye ndiye Musa, Firauni atamfuatilia kumkamata, walio pamoja naye watazingirwa na hofu na watasema ewe Musa, tumekamatwa na wakati huo Musa atasema kwa sauti kubwa: Kallaa inna ma'iya Rabbii sayah diini, hiyo haiwezekani kabisa, Mungu yu pamoja nami.

Kama Ruya yangu hii iliyokwisha chapishwa ndani ya gazeti la Al Fazal pia iunganishwe na Ilhaam hizo mbili, ambapo nilijiona nimo ndani ya nyumba fulani. Wakati huo nikajiwa na wazo moyoni mwangu kwamba hata nabii Musa pia aliwahi kuchukua hifadhi ndani ya jengo hilo. (Al Fazal jal. 32, uk. 142 tarehe 20 June 1944).

Hivyo, yafahamika kwa uwazi kabisa kwamba hiyo ni bishara ihusikanayo na siku zijazo ambayo itatimia kwa kupitia Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa kwa mdhihiriko mwingine wa *Layaalin 'ashrin*, yaani katika usiku wa tarehe 11 ulio sambamba na karne ya kumi na tisa. Na tukio fulani lifananalo na lile la kuokolewa Musa huko Misri litatukia kwa Jumuiya ya Ahmadiyya.

Sasa tutazame jinsi bishara hizi zilivyokuja timia katika historia ya Ahmadiyya. Mnamo tarehe 26 April 1984, Zia ul Haq, aliyekuwa mtawala wa kijeshi wa Pakistan mwenye sifa zote za kidikteta kama alivyokuwa Firauni, alitunga sheria ya kuwakandamiza Waahmadiyya na kuwakataza kujiita Waislamu, kutojifananisha na Waislamu, kutotoa Adhana kwenye misikiti yao na adhabu iliyowekwa ilikuwa ni ya kifungo cha miaka mitatu au faini au vyote kwa pamoja. Hapo hapo kukawa na mpango wa siri wa kumkamata Hadhrat Khalifatul Masih wa 4 rh.a. kisha auawe ndani ya siku tatu. Msaada wa Mungu uliteremka kwa namna ya ajabu na Hadhrat Khalifatul Masih IV rh.a. akafanikiwa kukimbilia Uingereza juu ya ulinzi mkali uliowekwa wa kumkamata. Baadae, mnamo mwaka 1988, Hadhrat Khalifatul Masih IV rh.a. akalazimika kutoa changamoto ya Mubahala kwa Zia ul Haq, ambaye jina lake likiwa ndio la kwanza kwenye orodha, ya kuomba dua kwa Allah ili laana ya Allah iangukie upande wa waongo kati ya Ahmadiyya na wapinzani wao.

Alilazimika kufanya hivi baada ya kuona Zia ul Haq anazidi kwenye utukutu na dhulma dhidi ya Waahmadiyya. Alimtahadharisha mara kadhaa aachane na dhulma dhidi ya Waahmadiyya lakini ndio kiburi chake kikawa kinazidi kupanda. Alikuwa na hasira kubwa sana ya kumkosa Khalifatul Masih juu ya ulinzi mkali aliouweka wa kumzuia asitoke nje ya nchi. Kwa hiyo hasira zake akawa anazimalizia kwa Waahmadiyya.

Huzur akaamua kufanya maombi makhsus kwa Mwenyezi Mungu kwa siku arobaini mfululizo na mnamo tarehe 10 June 1988 akatangaza dua ya Mubahala dhidi ya wapinzani wake. Khalifa Mtukufu rh.a. akaonyeshwa ruya fulani na Mwenyezi Mungu ambapo alionyeshwa kinu kikubwa cha kusaga kikiwasaga tikitiki na mnamo tarehe 12 Agosti 1988, kwa msingi wa ndoto hiyo, akatangaza ndani ya hotuba ya Ijumaa, yale aliyofunuliwa na Mwenyezi Mungu kuhusiana na Zia na majeshi yake, na kusema kwamba : 'hatima ya Zia imeshakaribia sana na sasa hakuna nguvu yoyote duniani itakayoweza kumuokoa na mwisho wake mbaya. Huzur pia alisema kwamba maangamio yatakayomkuta Zia hayatakutwa na mkono wa mtu ndani yake, bali itakuwa ni adhabu moja

Endelea uk 11

Bustani ya Washairi

DUNIA HAINA USAWA.

Mambo mengi yatendeka, Ya siri na hadharani,
Dunia imejiweka, kujizungusha juani,
Watu wake wateseka, Hususani masikini,
Dunia iliyoumbwa, Ikaumbika ikawa.

Ikawa na matabaka, Ya juu chini na kati,
Wapo wenye mamlaka, Wao shida hawapati,
Wanyanyasa vibaraka, Kwa binafsi mikakati,
Dunia iliyoumbwa, Ikakosa na usawa.

Usawa wa Binadamu, Nchi miji na wanyama,
Kila mtu ana hamu, Kileleni kusimama,
Walo nacho hudhulumu, Wasonacho hutetema,
Dunia iliyoumbwa, Ilojawa na maovu.

Maovu ya kuchukiza, Ya muudhio Muumba,
Wazungu wanajikweza, Masanamu kuyaumba,
Mwenyezi wa mchukiza, Wajisifuo kuumba,
Dunia iliyoumbwa, Na mwisho itafikia.

Na mwisho nimefikia, Wa mimi kuelezea,
Mambo yaliyotukia, Na yanayo endelea,
Katika hii Dunia, Bila ya kuongopea,
Dunia iliyoumbwa, Kwa Mola itarejea.

Abubakary Abdallah Mwita.
Mkurya halisi.

NDOTONI

Miluzi mingi jangwani, Angani naangalia
Ndege weupe fidhani, Mawingu waelea
Sikuamini machoni , Yale nayo shuhudia
Inaningia rohoni, Furaha nisotarajia

Nakodoa mboni zangu, Naona nyota ya jaha
Lo! Ufalme wa mbingu, Nazona fukwe za uraha
Komamanga na makungu, Najilia kwa madaha
Inaningia rohoni, Furaha nisotaraji

Mara napewa furushi, mbegu zisizo turufu
Kuzimbanda zashawishi, Ni ushindi yakinifu
Tamu ladha hainishi, ya pili yaja tukufu
Zote zafanywa tumishi, Ndoto nyemi natangaza

Shunda Mshundia Wana
Daluni, Tanga
+255656557721

DUNIA NAPITA

1. Inna lillahi Wa inna, ilayhi rajiun,
Sisi sote Wa rabbana, kwake ni marejeoni,
Ipo siku muungwana, taingia kaburini,
Si kupumbaze maisha, ya dunia yanapita.

2. Mola amefafanua, kwa mifano ya bayani,
Kwanamna kachambua, kwenyenjema furqani,
Ili tupate tambua, maisha ya duniani,
Si kupumbaze maisha, ya dunia yanapita

3. Sikio nakuazima, mfano ufikirini,
Khabiru alo usema, kwenye sura ya dhununi,
Akaeleza kwa kima, safari ikaribuni,
Si kupumbaze maisha, ya dunia yanapita.

4. Maisha ya duniani, kama mvua mbinguni,
Ikanyesha ardhini, ikastawi bustani,
Zikamea zeituni, kijani zuri ardhini,
Si kupumbaze maisha, ya dunia yanapita.

5. Uzuri ukavutia, Maji kapita mtoni,
Ndege wakausifia, kwa nyimbo za shukrani,
Nyuki katika maua, malighafi mkononi,
Si kupumbaze maisha, ya dunia yanapita.

6. Mwenye Shamba lipoona, akajisifu shambani,
Kasahau subhana, kutotoa shukrani,
Mwenye Nguvu kajiona, majigambo mdomoni,
Sikupumbaze maisha, ya dunia yanapita.

7. Alipolala usiku, alazizi mwenye shani,
Haukupita usiku, akaifyeka bustani,
Ikakauka kwa siku, akabaki majutoni,
Sikupumbaze maisha, ya dunia yanapita.

8. Kipi ulichojifunza, kwa mfano kitabuni,
Mungu aliotufunza, ili tupate yakini,
Ya dunia takuponza, mchezo mwisho motoni,
Si kupumbaze maisha, ya dunia yanapita.

9. Kwa witiri nasimama, Namba pendwa kwa manani,
Tujipange kwa qiyama, siku ya haki mizani,
Kifo hakina kukwama, hata uwe jabarini,
Si kupumbaze maisha, ya dunia yanapita.

Masihi Omary Kisagwa

MWANA ALIYEAHIDIWA

1. Salamu alaikumu, ndugu zangu waumini
Ama bada ya salamu, hongera ninawapeni
Kuhudhuria kalamu, siku njema ya amani
Mola Mjaze shufaa, Mwana Aloahidiwa

2. Ni ahadi ya manani, kwake Ghulam Miriza
kutujazia imani, kwa wote wanaoweza
wengi tumeshabaini, ukweli aloeleza
Mola Mjaze shufaa, Mwana Aloahidiwa

3. Alifika kwa wakati, Mola Alompangia
akiwa na mikakati, Jamati kuipanua
malengoye madhubuti, pande zote za dunia
Mola Mjaze shufaa, Mwana Aloahidiwa

4. Akiwa bado Khudamu, kazi akaianzia
lengole kwa wanadamu, Masihi kumtambua
mabara zamu kwa zamu, akianzia Asia
Mola Mjaze shufaa, Mwana Aloahidiwa

5. Kazi ya Mola Manani, alifanya kwa juhudi
kuzisafisha imani, ndiyo kubwa ya juhudi
wabaya nao wahuni, kuwapunguza idadi
Mola Mjaze shufaa, Mwana Aloahidiwa

6. Kwa usitadi mzuri, kaijenga Jumuiya
kuyaondoa mapori, mioyoni mwa insia
alikuwa muhisani, Jamati kuitetea
Mola Mjaze shufaa, Mwana Aloahidiwa

7. Tulifikwa na huzuni, majonzi yalotufika
kiongozi wa imani, buriani kaondoka
kaondoka duniani, karejea kwa Rabuka
Mola Mjaze shufaa, Mwana Aloahidiwa

8. kaliacha duniani, kundi la wenye vipawa
wasiopenda utani, Isilamu kuchezewa
mapepo na maruhani, mbali yatatupiliwa
Mola Mjaze shufaa, Mwana Aloahidiwa

9. ombi langu moja kwenu, enyi mnaosikia
Jumuiya kwetu tunu, Mola Alotupatia
Tusije kuwa bunumi, Jamati kupotezea
Mola Mjaze shufaa, Mwana Aloahidiwa

10. Tamati natamatia, mwishoni nimefikia
beti kumi naishia, kitini ninatulia
sifa njema twafatia, za Mwana wa Mahadia
Mola Mjaze shufaa, Mwana Aloahidiwa

Isihaka A. Nyamihasi,
SLP 54, Tabora

Hongera

Hongera nakutolea, kwa wako mwema utungo
Hakika metuzindua, kwa yako mema malengo
Memlenga Mwahidiwa, mazuri yake malengo
Karibu tena mwakani, utungo kututungia
H. R. Bundala,
Kiloleni, Tabora

N.B. Shairi hilo liliandikwa na kijana wetu mtajwa hapo juu na kusomwa naye siku ya Maadhimisho ya Mwana Aliyeahidiwa ambaye anatarajia kumaliza kidato cha sita (6) mwaka 2021 katika shule ya Ali Hasani Mwinyi, Tabora.

MODO

1. Enyi ndugu waungwana, tunakumbushana tena
Wala sio kusemana, moyo wangu unanuna
Nguo zetu za kubana, wala hazina maana
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

2. Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa
Vijana wamedhikika, na zinawabana hasa
Embu anza kukumbuka, usiziwaze anasa
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

3. Mavazi yaliyobana, wanavaa wanawake
Kama waona hiyana, kazana ubadilike
Sisi sote ni vijana, tusizidishe makeke
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

4. Zipo zenye kuchanika, magoti kuonekana
Na pia zenye viraka, tena zinapendwa sana
Miili zimewashika, hata pa kuhema sina
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

5. Wanapiga makelele, wanapofundishwa dini
Ujana kuweka mbele, dini ndio kitu gani?
Kazi kupiga misele, mwendo modo ya dukani
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa

6. Chini wanaweka zipu, ili ibane vizuri
Ukiingia upupu, utaipata habari
Waweza baki mtupu, ebu fanya tafakari
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.
7. Mara kuna mpauko, mara kamatia chini
Zunguka huku na huko, kuzunguka madukani
Usijepata anguko, kuanguka hadi chini
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa

8. Nguo yako mekubana, na unashindwa kuhema
Si vizuri we kijana, usiishi kama Kima
Rukia miti kwa sana, kuko wazi huko nyuma
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

9. Na Modo zenye majina, mara Bosi mara Zara
Hakuna kitu hakuna, wanafanya biashara
Vaa nguo za maana, na usifanye papara
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

10. Mnisameheni sana, nimewasema vijana
Bado tutakumbushana, Wahenga wanatuona
Hata kama mkinuna, na mbavu zikikubana
Eti modo kumodoka, ndo mavazi ya kisasa.

Abdallah Kalindima (K-mtoto)
#MMAKONDE MSOMI
kalindimasenior@gmail.com

DUNIA DANIYA

Katika tamthilia yake maarufu ya Juliasi Kaisari, William Shakesphere anatuonyesha Brutasi rafiki pete na kidole na Siza akinichoma kisu. Siza amepigwa na butwaa hata nawe Brutasi!? Kumbe *kikulacho....*

Shangwe na vigelegele, huweza kukuhadaa!
Ukamba u mteule, wote wakushangilia
Siza wa enzi za kale, kilio katuachia
Hata nawe Burutusi, Ai! dunia daniya

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)

Kisa cha Vyura

Kundi la vyura lilikuwa likirukaruka kwa kushindana vichakani, wakati wakielekea katika harakati zao za uchura chura, ndipo wawili kati yao walipoangukia katika shimo lenye kina. vyura wengine wote wakazunguka lile shimo kuona nini kinaweza kufanyika kuwasaidia wenzao. Walipoona namna shimo lilivyo refu, wakapatwa na fadhaa na kukubaliana kuwa hakuna tumainio na kuwaambia wale vyura wawili kwamba wajiandae tu kukutana na mwisho wao, maana walikuwa kama maiti tu.

Wakiwa hawako tayari kukubali mwisho wao huo mbaya, vyura wawili walianza kuruka kwa nguvu zao zote. Baadhi ya vyura walipiga kelele shimoni kwamba ilikuwa kazi bure, na kwamba wale wawili wasingekuwa katika hali ile endapo wangekuwa makini zaidi, watiifu zaidi kwa sheria za vyura, na kuwajibika zaidi.

Vyura wengine waliendelea kutoa sauti kwa huzuni wakiwaasa kuokoa nguvu zao na kukata tamaa, kwani walikuwa ni wa kufa tu. Vyura wawili waliendelea kuruka kwa nguvu kadri walivyoweza, na baada ya saa kadhaa za juhudi endelevu walikuwa wamechoka hoi.

hatimaye, mmoja wa vyura akakubaliana na shauri la vyura wenzake. Akiwa hoi na amekata tamaa, akajikatia shauri kwenye mwisho wake, akalala kwenye kina cha shimo, na akafa wakati wengine wakimtazama kwa huzuni ya kutojiweza. Chura mwingine aliendelea kuruka kwa kila lepe la nguvu alilokuwa nalo, licha ya kuwa mwili ulichakazwa na maumivu na hoi taabani.

Wenzake wakaanza upya, wakimpayukia kukubali hali yake, "acha kujiumiza wewe kufa tuuu!". Chura yule aliyechoka akaruka kwa jitihada zaidi na zaidi na - maajabu ya dunia! Hatimaye akaruka juu sana kiasi kwamba akachopoka kutoka shimoni. Wakiwa



wamestaajabu, vyura wengine walishangilia uhuru wake wa kimaajabu na wakamzunguka wakimuuliza, "Kwa nini uliendela kuruka wakati tulikuambia kwamba haikuwezekana?" Akisoma midomo yao, chura aliyeshangazwa aliwaelezea kuwa alikuwa kiziwi, na wakati alipokuwa akiona ishara na makelele yao, alifikiria wanamshangilia. Alichofikiria kama kutiwa moyo kilimpa kariha ya kujaribu zaidi na kufanikiwa dhidi ya magumu yote.

• • • •

Utengezaji wa Kashta za Ubuyu

Na **Mtandao**



Mahitaji:

- Unga wa ubuyu 1/2
- Sukari 1/4
- Rangi kijiko 1 cha chakula
- Vanilla kifuniko 1
- Maji vikombe 2
- Pilipi manga

Jinsi ya kuzipika

i. Chukua unga Wa ubuyu chekecha upate ule mzuri na safi.
ii. Kisha weka maji yako jikoni tia sukari, Rangi, vanilla na pilipili manga.
iii. Koroga mpaka uone mchanganyiko wako unatoa povu na ukigusa unanata.
iv. Weka unga wako, anza kusonga kama ugali hivi.
v. Andaaa sinia, paka mafuta epulia hapo kisha usukume na sukumio la chapati, kisha kata mtindo uupendao.

Furahia kashata za ubuyu.

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA^{AS}

Kuwasingizia Wengine

Kusingizia na kunasibisha dhana mbaya juu ya matendo ya watu wengine ni maradhi na dhamira mbovu nafsini mwa mtu inayochafua uzuri wa imani yake na utawa na huiunguza kwa haraka kama vile moto uunguzavyo majani makavu. Zama wauguao maradhi hayo wawafanyapo Manabii shabaha za mashambulio yao na kuwasingizia, Mungu huwa adui wao Naye Huwalinda Manabii Wake. Hulinda heshima ya wapenzi Wake kwa ghera isiyo na kifani. Nilipozozwa na kushambuliwa kwa njia mbali mbali, ghera hiyo hiyo ya Mungu ikawa ngao ikajitokeza kunilinda.

(Roohani Khazain Jal. 20: Al-Wasiyyat Uk. 26 maelezo)

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

Haja ya Nuru ya Allah

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

*Na hushughuliki katika kazi yo yote, wala husomi humo katika Qur'an, wala hamfanyi kitendo cho chote, isipokuwa Sisi Tunakuwa mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo. Wala hakifichikani kwa Mola wako kitu cho chote kilicho sawa na uzito wa chembe katika ardhi wala katika mbingu, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa, isipokuwa kimo katika Kitabu kielezacho. (*Sura 10:62)

NURU ni mwanga wa Muongozo. Nuru huhitajika kwenye Kuona na Kusikia na Kuhisi. Mwanadamu amejaliwa Mwanga wa kuonea na Sauti ya usikia na vitu vyenye kutoa Hisia. Sawa na mahitaji ya mwanadamu Mwanga aliojaliwa na Sauti zote na Vitu vyote alivyopewa bado anahitaji zaidi Nuru. Mwanga na sauti na vitu vyote vimewekewa Ukomo wa Mdogo au Mkubwa.

Maneno haya ASGHAR na AKBAR (kidogo na kikubwa), yametumiwa kuonyesha ya kwamba, kuna baadhi ya vitu vinafichikana kwa sababu ya udogo wao, na kuna vingine vinakuwa vikubwa sana hata kwa kiasi cha kufanya sehemu zao nyingine zisionekane. Kwa mfano, mtu anaweza kuona sehemu tu ya mlima mkubwa wala si wote. Kwa hiyo Qur'an inasema sawa ya kwamba nguvu ya kuona ya Mwenyezi Mungu ni kali kabisa hata hakuna kitu kiwe kidogo namna gani kinaweza kufichama asikione. Na pia nguvu Yake ya kuona imeenea kabisa hata kitu kiwe kikubwa chapataje hakuna sehemu yake yo yote itakayokaa asiione.

Kadhalika elimu ya sayansi imehakikisha ya kwamba kuona na kusikia kunategemea mitingisho yenye kikomo. Kuna kikomo cha jicho kuona na sikio kusikia. Nguvu ile inapopungua au kuzidi kiasi kinachotakiwa, jicho halitaona wala sikio halitasikia. Kwa mfano, sikio haliwezi kusikia sauti iliyo si chapu chapu kuliko mitingisho thelathini kwa nukta moja; wala haliwezi kusikia sauti iliyo kasi zaidi ya mitingisho arobaini kwa nukta moja. Hivyo, hata elimu ya sayansi imehakikisha ya kwamba baadhi ya vitu vinaliponyoka jicho au sikio kwa sababu ya ima udogo wao au ukubwa wao. Lakini Qur'an inasema, hivyo sivyo mambo yalivyo kwa Mwenyezi Mungu ambaye anaviona vitu vyote kwa ukamilifu, vidogo au vikubwa.

Licha ya uvumbuzi wa vyombo mbalimbali ila uwezo wake mwisho kwenye atom ndogo ndio anaweza kuona au kusikia. Wakati mahitaji yake yapo zaidi ya hapo. Mfano dereva anaweza kuwa amepimwa ana akili timamu, afya nzuri, kiwango chake cha uchovu kipo vizuri, hana pressure wala stress, gari nzuri na mbalimbali nzuri na hadhari zote zikachukuliwa za ajali ila ajali akapata ni kuwa kuna vitu mwanadamu hanauwezo navyo ambavyo vyote hivyo vikiitaji Nuru ya Allah. Nuru hii inapofika au kuwa nao huondoa giza linalokutanda 57:10 ila unapoimiliki basi huo Muongozo wako wa kila jambo 57:13

Haja ya Nuru ya Allah ni kuwa tafsiri ya Elimu zote za mwanadamu ni kwenye matendo na vitu yaani kuwepo kitu au kitendo ndipo ajue, aone au asikie. Na ndivyo elimu yake imeanzia kwenye "atom" wakati Elimu hainzii kwenye Atom ila kwenye ujinga - hakuna ndipo atom ikapatikana. Hii hakuna ni Giza la watu wote. Ili Elimu zetu na mipango yetu iwe na maana basi tunatakiwa kuanzia kwenye hii Nuru ya Allah. Maana licha ya Elimu dunia ilipofikia bado haina Uhakika wa kesho yake. Bado mipango yetu haifikiwi kwa kiwango cha asilimia mia moja ni mfano tu kwa Daktari amefikia kiwango cha kuamini wao Hutibu ila hawaponyeshi mwenye Kutibu ni Mungu. Wachumi hawana uhakika na uchumi wao ambapo husema uchumi unadesturi ya kupanda na kuanguka. Na ndivyo Mwana Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Bashirudin Mahmood Ahmad^{ra} akiwa na umri mdogo Madaktari wakasema hana umri mrefu atakufa na akaja kuishi maisha mrefu kuliko hata umri wa Mtume^{saw} na hata alipochomwa kisu madaktari wakamwambia maisha yake hayatakuwa marefu ila Mwenyezi Mungu Akamwambia Kisu hicho hakitakuuwa na aliishi na Kipande cha Kisu kwenye mshipa mkuu wa Fahamu kwa miaka 21 kabla ya Kufariki. Nuru hii inapatikana kwa kuungana na Mwenyezi Mungu na njia mojawapo ni Ibada na njia yake kuu ya Ibada ni Sala.

Mtume^{saw} alisema katika hadithi iliyosimuliwa na Hazrat Abu Said^{ra} ya kwamba: Iogopeni busara ya Muumini, kwani yeye anaona kwa Nuru ya Allah.... ***Tirmidhi***

Leo hii dunia inashuhudia Elimu mbalimbali zikivumbuliwa ikiwa kwa sababu ya Hekima ya Quran Tukufu na Mtume^{saw} ni kwa sababu ya Uwepo wa Masih Aliyeahidiwa a.s na Makhalifa wake na Watakatifu mbalimbali waila dunia ingebaki bado Gizani. Ndivyo Allah Anavyosema:

*Yeye ndiye Anayeteremsha Ishara zilizo wazi juu ya Mtumishi Wake ili kuwatoeni katika giza mwende kwenye nuru, na bila shaka Allah ni Mpole kwenu. Mwenye rehema. (*Sura 57:10)

Mola wetu, Ututimizie nuru yetu, na Utughofirie; hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu. Amin

MATUKIO KATIKA PICHA




Wanajumuiya wa Mwanza wakifanya Wakal Amal kwa kusafisha maeneo ya Hospitali ya Bohongwa kwa kufagia, kukata nyasi na kutengeneza njia.



Wanajamaat wakifanya Waqar-e-Amal kwa kusafisha barabara na baadhi ya eneo huko Maungani, Zanzibar.

1



2





3



4





Ibada ya Idi-el-Adhha Jamaat ya 1. Kivule, 2. Tegeta, 3. Mnazi Mnoja na 4. Jamia,

Jamaat Zanzibar wakiuza vitabu katika Idi-el-Adhha



Wanafunzi wa Jamia Ahmadiyya Tanzania wakishiriki katika kipindi cha malezi wakipata nasaha kuhusu uhakika wa Majini, Uchawi na Ramli.





Mikutano ya malezi Jamaat za Mitonga na Butibu, Shinyanga.



Mbashiri wa Arusha, Sheikh Muhammad Shafi Memon akiwapa mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya - Arusha zawadi ya vitabu aliposhiriki mkutano wa viongozi wa dini mkoani humo.



Sheikh Bashart ur Rehman akisaini kitabu cha rambirambi cha msiba wa Rais Mstaafu Benjamin William Mkapa nyumbani kwake.

Seyidna Ahmad as Mjini Sialkot



Sheikh Muzaffar Durrani
Rabwah, Pakistan

SEYYIDNA AHMAD as. ALIPOKAA MJINI SIALKOT KATIKA UJANA WAKE

(Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani)

Seyyidna Ahmad as. Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya katika ujana wake, alipolazimishwa na baba mzazi kufanya kazi basi alienda huko mjini Sialkot kufanya kazi katika ofisi ya Serikali kwa miaka michache 1864-1868. Hakuridhishwa na kazi hiyo, hata hivyo alimtii baba yake. Alitaka kutumikia dini ya Mungu tu, hiyo ni sababu kwamba alipoulizwa kwamba je unaipenda kazi hii? Akasema: "Ni gereza tu." Leo nitawaelezeni baadhi ya matukio ya maisha yake ya zama zile.

TUKIO LA KIMWUJIZA LA HIFADHI YA MUNGU

Baada ya kufika Sialkot, kwanza kabisa alilazimika kukaa katika ghorofa moja katika mtaa wa Jhandanwala. Akielezea tukio la ghorofa hiyo kuanguka na kusalimika kimwujiza kwa wenzake wote waliokuwamo ndani kwa sababu yake; anasema: "Usiku mmoja nilikuwa nikilala ghorofani mwa nyumba moja, na katika chumba hicho watu 15 au 16 pia walikuwa pamoja nami. Wakati wa usiku sauti ya "tik-tik" ilisikika boritini, nikawaamsha watu kwamba boriti hii ni hatari, inapaswa tuondoke hapa. Wakasema, labda ni panya tu; hakuna jambo la hofu na wakalala tena. Baada ya muda kidogo tena sauti kama hiyo ikasikika, ndipo nikawaamsha tena lakini hawakujali. Kisha mara ya tatu sauti ikasikika katika boriti hapo nikawaamsha kwa nguvu na kuwatoa wote nje ya nyumba. Na walipokwishatoka wote, nikatoka mwenyewe. Nilipokuwa kwenye kipago cha pili cha ngazi, mara paa likaporomoka, na likaanguka chini pamoja na paa la pili, na wote wakasalimika." (Siratul Mahdi, sehemu ya 1, uk. 236)

UTAWA WA SEYYIDNA AHMAD as.

Shamsul Ulamaa Maulana Seyyid Mir Hasan marehemu, juu ya kukaa mjini Sialkot kwa Seyyidna Ahmad as. Kabla ya madai yake, anasema:

"Hadhrat Mheshimiwa Mirza alikuja mjini Sialkot kwa ajili ya kufanya kazi na alikaa huko mnamo mwaka 1864. Yeye alikuwa akipenda kukaa peke yake, alikuwa mtawa na alitengana na mambo yasiyo na maana, kwa hiyo alikuwa hapendi kukutana na watu wa kawaida, jambo ambalo mara nyingi linasababisha kupoteza wakati.

Watu wa mahakamani hawakujua utaalamu wa Bwana Mirza. Mwaka huo huo kijana mmoja Mwarabu, jina lake Muhammad Salih, aliwasili mjini na akadhaniwa kuwa jasusi. Basi Mkuu wa Polisi aitwaye Bwana Harcison (ambaye baadaye akawa Kamishna wa Rawalpindi) alimwita Muhammad Salih katika ofisi yake kwa upelelezi. Basi, akahitajika mkalimani. Kwa kuwa Bwana Mirza alijua sana Kiarabu na aliweza kuandika na kusema vizuri kwa lugha ya Kiarabu, kwa hiyo yule ofisa akamwita Bwana Mirza na kumwambia amwulize Mwarabu nitakayomwuliza na kuandikisha majibu yake kwa Kiurdu. Bwana Mirza aliifanya kazi hii ipasavyo, na hivyo umahiri wake ukajulikana kwa watu.

Siku hizo Chuo cha Panjab kilianzishwa, humo mwalimu wa Kiarabu alihitajika kwa mshahara wa Rupia 100. Nilimwambia, upeleke ombi la kupatiwa nafasi hii maana ujuzi wako wa lugha ya Kiarabu ni kamili sana, kwa hiyo lazima utapewa kazi hii. Akajibu, sipendi kazi ya ualimu, kwani watu wengi baada ya kusoma wanafanya kazi za ukorofi sana na wanaitumia elimu kuwa njia ya kufanya kazi zisizojuzu. Naogopa sana onyo la aya hii: اُحشُرُوْا الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا وَ اَزْوَاجَهُمْ Yaani wakusanyeni wale waliodhulumu na wenzao. (Assaaffaat 37:23) Jibu hili linaonyesha kwamba alikuwa mtu mwema sana.

Safari moja mtu mmoja alimwuliza kwamba kwa nini manabii hawatokwi na manii usingizini? Akasema, kwa vile muda wote, wakilala au wakiamka, manabii huwa na fikara takatifu na hawaziruhusu fikara chafu kuingia moyoni kwa hiyo hata katika ndoto hawapati kutokwa na manii.

Safari moja, ilipokuwa inazungumzwa kuhusu mavazi, mtu mmoja akasema kwamba pajama lenye nafasi pana za kupenyezea miguu huwa bora. Hapo Bwana Mirza alisema kwamba pajama lenye nafasi ndogo ya kupenyezea mguu ni bora na afadhali kwa kujisitiri, na inasitiri vizuri zaidi, kwani kwa kuwa nafasi hiyo ndogo inasitiri hata kwa ardhi pia. Wote wakapenda jibu hili.

Hatimaye, akivunjika moyo alijiuzulu kazini na akaondoka hapa mwaka 1868. Safari moja akaja hapa mwaka 1877 na alikaa nyumbani mwa Lala Bhiim Sain, na akaja nyumbani kwa Hakiim Mir Husamuddin alipoalikwa. (Siratul Mahdi, sehemu 1, uk. 54 chapa ya kwanza.)

USHAHIDI WA PILI

Shamsul Ulamaa Maulana Seyyid Mir Hasan marehemu katika ushahidi wake wa pili anasema:

"Hadhrat Mirza alikaa nyumbani mwa Umra Mkashmiri akiwa mpangaji karibu sana na nyumba yangu katika mtaa wa Kashmirian. Baada ya kurudi kutoka mahakamani, yeye alikuwa anashughulikia kusoma Qur'ani Tukufu. Akasoma Qur'ani akikaa, akisimama na akitembea na akalia sana. Akasoma Qur'ani kwa unyenyekevu na uchungu usio na kifani. Jinsi ambavyo wenye haja sawa na mazoea ya zama wanawaendea maofisa, hivyo ndivyo walivyokuwa wakimfikia yeye pia. Kaka wa Umra aliyeitwa Fadhl Din alikuwa mwenye heshimiwa katika mtaa ule, Bwana Mirza alikuwa akimwita na kumwambia, Mian Fadhl Din! Wafahamishe watu hao wasije hapa, wasipoteze wakati wao na wangu, siwezi kufanya chochote, mimi si hakimu. Kazi yote inayohusikana nami nilimaliza kule kule mahakamani. Bwana Fadhl Din alikuwa akiwafahamisha watu hao na kuwaondoa. Maulawii Abdul Karim ra. pia alizaliwa katika mtaa huo na kukulia na akawa kijana, na hatimaye akawa miongoni mwa waliomkurubia Bwana Mirza.

Baadaye yeye alikaa katika sebule moja iliyotazamana na msikiti wa Ijumaa pamoja na Mansab Ali Hakiim aliyekuwa na cheo cha heshima cha kuwa mwandishi wa hati. Karibu na sebule alikuwa mzee moja mwenye duka, jina lake Fadhl Din, aliyekuwa analala usiku dukani tu. Marafiki zake wengi walikuwa wakija kwake baada ya jioni, wote walikuwa watu wema. Wakati mwingine Bwana Mirza pia alikuwa akija huko, na mara moja moja Bwana Nasrullah Mkristo pia akaja aliyekuwa mwalimu mkuu wa shule ya Misheni. Mara nyingi Bwana Mirza na mwalimu mkuu walikuwa wakijadiliana juu ya mambo ya dini. Watu walikuwa wakifaidika na hotuba ya Bwana Mirza.

Kulikuwa na mzee mmoja mtawa sana, mwema, asiyependa anasa za dunia, jina lake Maulawii Mahbub Aalam, ambaye Bwana Mirza alikuwa akimtembelea na alikuwa akimsisitizia Lala Bhiim Sain pia kuwa awe anamtembelea Bwana Maulawii huyo. Kwa hiyo, yeye pia wakati mwingine alikuwa akimtembelea. Kila ilipotajwa baiati na uongozi na ufuasi. Bwana Mirza alikuwa akisema kwamba inampasa mtu afanye mwenyewe bidii. Kwani Mwenyezi Mungu Anasema:

وَالَّذِيْنَ جَاهَدُوْا فِيْنَا لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبُلَنَا Yaani na wale wanaojitahidi kwa ajili yetu, kwa yakini Tunawaongoza kwenye njia zetu. (Sura Al-'Ankabut, 29:70)

USHINDI KATIKA MBIO

Bwana Seyyid Mir Hasan anaendelea kusema:

Ni dhahiri shahiri kuwa Bwana Mirza aliwatangulia wote katika elimu ya dini, lakini katika mbio za kidhahiri pia ushindi wake ulithibitika kwa uwazi juu ya watu wa wakati ule.

Maelezo yake ni hivi kwamba safari moja baada ya kumalizika saa za kazi za mahakama, wafanyakazi wakaanza kurudi nyumbani, hivi tu ilitajwa kukimbia kwa kasi na shindano la mbio. Kila mmoja alidai anaweza kukimbia sana. Hatimaye, Singasinga mmoja, aitwaye Billa Singh, alisema kwamba ninawashinda wote katika mbio. Hapo Bwana Mirza alimwambia, "Shindana nami katika mbio, basi itathibitika nani anakimbia sana." Hatimaye, Sheikh Allah Dad aliwekwa kuwa mwamuzi, na ilipangwa kwamba wakimbie bila viatu kuanzia hapa mpaka daraja ile inayotenganisha barabara ya mahakama na mji. Mtu mmoja lishika viatu vyao na mtu mmoja alitumwa mapema aende pale darajani ili atoe ushahidi nani ameshinda na ametangulia kufika kwenye daraja. Bwana Mirza na Billa Singh walianza kupiga mbio wakati mmoja. Watu wengine walitembea nyuma yao kwa mwendo wa kawaida. Walipofika kwenye daraja ikathibitika kwamba Bwana Mirza alishinda na Billa Singh alishindwa." (Siratul Mahdi, sehemu 1, chapa ya pili, uk. 270-272.)

Habari za Ghaib Zadhihirisha Ukweli wa Ahmadiyya

Kutoka uk. 5

kwa moja toka kwa Mwenyezi Mungu. Inasemekana kwamba siku chache tu baadae, Zia aliwakusanya masheikh wengi na kuwaahidi kwamba akirejea kutoka kwenye safari yake ya Bahawalpur basi hapo ndipo atakapowashughulikia Waahmadiyya barabbara akiwa amechukizwa na tambio la Mubahala dhidi yake toka kwa Hadhrat Khalifatul Masih. Ilikuwa ndani ya mwezi wa Muharram, mwezi aliohiliki Firauni na majeshi yake, wakati Zia ul Haq alipopanda ndege yake ya Kirais akiandamana na majenerali zaidi ya thelathini ndani ya ndege hiyo hiyo moja, pamwe na balozi wa Marekani na afisa mwingine wa cheo cha juu wa ubalozi huo. Ilikuwa ni kinyume kabisa na itifaki, kwani haijawahi kutokea raisi apande ndege moja pamwe na majenerali wa jeshi zaidi ya thelathini pamoja na mabalozi wa Marekani, nchi iliyokuwa ikihamasisha kwa siri na kushinikiza kuwa sheria kandamizi dhidi ya Waahmadiyya zisiondolewe huko Pakistan, ikichelea isije wapakistan wakajiunga kwa wingi na Jumuiya hii na hivyo kuwa nchi isiyonyonyeka.

Mnamo siku ya Jumatano ya tarehe 17 Agosti (Muharram) 1988, ndege ya Zia ililipuka angani wakati ikirejea kutoka Bahawalpur na kuangukia karibu na mto wa Bahawalpur. Moto mkali uliwaka kwenye ndege hiyo na kuwateketeza wote waliokuwemo humo na kuwageuza majivu kabisa. Ni jino tu la dhahabu la Zia ndio lililosalimika na kuzikwa. Hivyo Firauni wa zama zetu, Zia ul Haq, pamwe na viongozi wa kijeshi wenye vyeo vya majenerali zaidi ya thelathini waliowakilisha majeshi yake na pia mabalozi wa Marekani waliowakilisha majeshi ya Marekani yaliyokuwa yakiwafadhili, wakahilikishwa ndani ya siku hiyo ya Jumatano ya mwezi wa Muharram, siku na mwezi aliohilikishwa Firauni katika zama za nabii Musa[as] kama inavyothibitishwa na Hadithi ile ya Mtume[saw]. iliyomo ndani ya kitabu cha Durrun Manthur cha Imam Suyutwi jalada la 6 isemayo kwamba Mtume Muhammad[saw]. alisema kwamba Mwenyezi Mungu Alimuangamiza Firauni na wenzake mnamo siku ya Jumatano na hali kadhalika ndani ya Kitabu cha Hadithi cha Jaamii Tirmidhi Kitabus swaum, bab ma jaa a fi swaumil muharram, kuna Hadithi iliyosimuliwa na Hadhrat Ali[ra] iliyodhihirisha kwamba ilikuwa ni ndani ya mwezi wa Muharram Mungu Alipowaokoa wana wa Israeli kwa kumuangamiza Firauni. Hali kadhalika Zia ul Haq naye aliangamizwa mnamo siku ya Jumatano ndani ya mwezi wa Muharram. Matukio haya hayawezi kuachwa yatukie kwa waongo kama wanavyodai akina Sawafi na wenzake. Mungu Awaongoze kwenye nuru. Amin

Watu Walio Bora Kabisa: Masahaba wa Badr

Kutoka uk.12

wale masahaba waliokuwa wanajeruhiwa vitani walikuwa wanawekwa kwenye mahema katika mazingira ya msikitini. Hata hivyo pamoja na utaratibu wa matibabu na uangalizi kwa hadhrat Sa'ad[ra] lakini hakuweza kupona. Naye katika usiku mmoja akafariki. Hadhrat Sa'ad bin Mu'az[ra] katika Maansar alikuwa na ubora uleule aliuokuwa nao hadhrat Abu Bakar[ra] katika Muhajirina. Yeye alikuwa na imani na mapenzi ya kweli kwa Mtume[saw], ikhlasi yake ilikuwa ya hali ya juu. Mapenzi yake kwa Mtume[saw] na dini ya Islam, yalikuwa yanadhihirika katika vitendo vyake. Yeye alikuwa ni chifu wa kabila lake pamoja na hayo heshima na unyenyekevu aliokuwa nao kwa Mtume[saw], kwa watu wa wakati ule mjini Madina ulikuwa mfano wa kuigwa na uliowapa athari kubwa. Kwa hiyo kufariki kwa mtu muhimu kama huyu ilikuwa ni jambo la lazima kwa Mtume[saw] kuhuzunika.

Kutokana na kifo chake, mama yake alikuwa anamlilia huku akitaja sifa zake njema. Mtume[saw] kwa kawaida hakuwa anapenda tabia ya kuwalilia watu kupita kiasi wanapokufa. Baada ya kusikia hayo Mtume[saw] alisema kwa kawaida watu wanaowalilia ndugu zao wanaokufa huwa wanapitiliza kutoa sifa hata zile za uongo lakini mama wa Sa'ad amezitaja sifa za kweli za Sa'ad.

Wakati wa kuzikwa kwake wanafiki walibeua jeneza lake wakisema mbona jeneza lake ni jepesi sana? Mtume[saw] alipopata taarifa hii akasema jeneza lile lilikuwa jepesi si kwa sababu ya makosa bali malaika elfu sabini (70,000) walikuwa wameshuka kuja kusaida kubeba jeneza lake na watu walioshiriki katika mazishi yake walikuwa ni wengi kiasi kwamba uwanja wa makaburi ya Janna tul Baki'i ulifurika na watu wengi.

Sayyidna Bi Aisha[ra] anasema kutokana na kifo cha hadhrat Sa'ad bin Mu'az Mtume[saw] alipata huzuni kubwa. Alipofariki alikuwa na umri wa miaka 37. Watu walipokuwa wanarudi baada ya kumzika, machozi yalikuwa yanadondoka kutoka kwenye sharafa za Mtume[saw].

Khalifa mtukufu[atba] anasema sahaba mwingine anayefuata ni hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas[ra]. Huyu alikuwa miongoni mwa wale masahaba ambao Mtume[saw] alitoa habari njema ya kuingia peponi wakiwa hai hapa hapa duniani. Na masahaba hao wote kumi walikuwa ni Muhajirina na Mtume[saw] alikuwa radhi nao muda wote mpaka anafariki.

Hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas anasimulia kuwa siku niliyojiunga na Islam hakuna mtu mwingine aliyefanya hivyo nami nilikuwa nimejiunga kabla sala haijafaradhishwa. Yeye anasema kuwa siku moja niliona ndoto. Sehemu zote zilikuwa giza hakuna kilichokuwa kinaonekana. Mara ukatokea mwezi unaong'aa, nami nikatembea kuelekea huko. Mbele yangu walikwepo hadhrat Zaid bin Harith[ra], hadhrat Abu Bakr[ra] na hadhrat Ali[ra].

Wakati ule Mtume[saw] alikwishadai kuwa Nabii na alikuwa anapokea bai'at kwa siri. Nami nilipoona ndoto hii nikahamasika kujiunga naye. Hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas[ra] alipojiunga na Islam baadhi ya watu wanasema alikuwa katika umri wa miaka 17 na wengine wanasema alikuwa katika umri wa miaka 19. Yeye alitokana na bani Zahara na mama ya Mtume[saw] pia alikuwa ametokana na kabila hili. Yeye alikuwa ni hodari na jasiri sana.

Yeye alipojiunga na dini ya Islam mama yake bado alikuwa ni mshirikina. Kwa sababu ya Islam alikuwa anamchukia na kumtesa mwanaye. Lakini hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas hakuiacha dini ya Islam na zaidi ya hayo aliendelea kumheshimu na kumuenzi mama yake kwa kumpa huduma zote sawa na dini ya Islamu inavyofundisha.

Mtume[saw] alikuwa anamwita mjomba wake. Mtume[saw] alikuwa anasema enyi watu nionesheni mjomba mwingine zaidi ya Sa'ad bin Abi Waqas.

Imam Tirmidhi anasema Mtume[saw] alikuwa anamwita yeye mjomba wake kwa sababu ya kutokana kwake na banu Zahara na mama yake (Mtume[saw]) pia alikuwa ametokana na banu Zahara.

Katika zama wakiwa Makka yeye alikuwa anasali pamoja na masahaba wengine sehemu fulani. Washirikina wakawaona na kuwafanyia istehzai na wakaizidisha kupita kiasi kwamba hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas alikasirika akampiga mmoja wao kwa mfupa wa ngamia kichwani mpaka akafa. Hii ilikuwa ni damu ya kwanza kumwagika baada ya kuja kwa Islam.

Katika kitabu cha ***Siratun Nabii*** imeandikwa kuwa yeye alikuwa miongoni mwa wale masahaba wa mwanzo waliopata mateso makubwa katika njia ya Mwenyezi Mungu. Yeye alikuwa miongoni mwa wale walioishi katika ***Sheebe Abu Talib***, naye alivumilia mateso mengi kwa ujasiri mkubwa. Baada ya kuhamia Madina Mtume[saw] aliweka udugu baina ya hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas[ra] na hadhrat Sa'ad bin Mu'az[ra].

Walipohamia Madina siku za mwanzo Mtume[saw] na masahaba zake walikuwa hawalali usiku kwa sababu ya hofu ya kushambuliwa na makafiri. Bi Aisha[ra] anasimulia kuwa Mtume[saw] siku moja alisema laiti nigempata mtu mmoja mwema wa kufanya ulinzi ili mimi niweze kulala. Muda si mrefu akasikia nje silaha zinagongana, akauliza wewe ni nani. Akajibu mimi ni Sa'ad. Akauliza wewe umekuja kwa sababu gani. Akajibu moyo wangu uliingia wasiwasi ya kwamba wewe uko katika hatari unahitaji ulinzi kwa hiyo mimi nimeamua kuja. Ndipo Mtume[saw] akaomba dua: Ee Mola wangu, Ujaalie mshale wake uweze kulenga na pia dua yake iweze kupokelewa. Naye alikuwa mashuhuri katika kupokelewa dua zake kwa sababu ya dua hii ya Mtume[saw].

Safari moja hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas[ra] alisingiziwa na mtu mmoja. Akaomba dua kwamba Mwenyezi Mungu ampofushe macho yake na kurefusha umri wake. Dua yake ikapokelewa mtu yule kweli akawa kipofu na akaishi katika mateso makubwa katika umri mrefu.

Katika zama za ukhalifa wa hadhrat Ali[ra], hadhrat Sa'ad bin Abi Waqas[ra] alimsikia mtu mmoja akimtukana hadhrat Ali[ra]. Akamwambia yule mtu, huyo hadhrat Ali[ra] unayemtukana yeye ni wa kwanza katika waaminio, yeye ni ndugu wa damu wa Mtume[saw], naye ni mkwe kwa Mtume[saw]. Ndipo alipoomba dua kwamba: Ee Mola wangu mimi nisiondoke hapa mpaka pale utakapoleta ishara yako. Alikuwa bado hajaondoka mara mtu yule akaanguka kutoka juu ya farasi wake na kupigiza kichwa chake kwenye jiwe na kufa pale pale.

Khalifa mtukufu[atba] anasema maelezo yake yataendelea katika hotuba ya Ijumaa ijayo. Baada ya sala nitaongoza sala ya jeneza ya watu watatu, na akazungumzia maisha yao ya sifa zao kwa ufupi.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Dh. Qd - Dh. Hj 1440 AH | JULAI 2020 | WAFA 1399 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu[saw]

Mtukufu Mtume Muhammad[saw] alisema: ***Mbora wenu ni ambaye ni mwema zaidi kwa kulipa deni.***

(**Kashful-Ghummah**).

Watu Walio Bora Kabisa: Masahaba wa Badr

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 17/07/2020 iliyotolewa Masjid Mubarak, Islamabad, UK; baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Amir ul Mu'miniin, Mirza Masroor Ahmad[atba] (**'A**yyadahullahu **T**a'ala **B**i-Nasrihil **A**ziiz') alisema;

Katika hotuba ya Ijumaa iliyopita habari za Hadhrat Sa'ad bin Mu'az[ra] zilikuwa zinaendelea kuelezwa. Kuhusiana na habari hii kisa cha vita vya Ahzab kimeelezwa katika kitabu cha ***Siratun Nabii***[saw] kuhusu hadhrat Sa'ad bin Mu'az[ra] hivi: Katika vita hivi Waislamu hawakuuawa kwa wingi. Hata hivyo hadhrat Sa'ad bin Mu'az[ra] majeraha yake aliyoyapata yalikuwa yenye maumivu makali kwa hiyo majeraha haya hayakupona na akafariki katika hali hii. Kufariki kwake hakukuwa na mbadala na hata upande ule wa makafiri pia ulipata watu wachache waliouawa.

Hadhrat Aisha[ra] anasimulia kuwa katika siku ya vita vya Ahzab nilimsikia hadhrat Sa'ad bin Mu'az[ra] akisoma mashairi ya kivita. Pindi hadhrat Sa'ad alipojeruhiwa mkononi Mtume[saw] mwenyewe aliuondoa mshale uliomjeruhi na akachoma kidonda kwa moto ili kisioze. Hadhrat Sa'ad alipopata majeraha haya aliomba: Ee Mola wangu usinipe kifo mpaka pale nitakapotimiza masuala ya Banu Quraiza.



Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V[atba] huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Mtume[saw] kwa ajili ya matibabu na uangalizi wa hadhrat Sa'ad bin Mu'az aliweka hema yake katika mazingira ya msikitini kwake. Majeraha yake yalipoanza kupona hadhrat Sa'ad[ra] akaomba: Ee Mola wangu kama vita baina ya Waislamu na makafiri itaendelea basi uendelee kuniweka hai, na kama vita haitaendelea basi lifanye jeraha langu lipasuke na kwa sababu yake mimi niweze kupata ushahidi (kufa). Kwa hiyo katika usiku ule ule jeraha lilipasuka na kutokwa na damu nyingi na akafariki. Kidonda kilipopasuka Mtume[saw] alipewa habari yake akafika kwake na akapakata kichwa chake mapajani pake naye akaomba: Ee Mola wangu Sa'ad amefanya jihadi katika njia Yako naye amethibitisha ukweli wa Nabii wako na ile kazi iliyokuwa jukumu lake ameitimiza, Basi upokee roho yake kwa kheri kama unavyopokea roha za watu wengine.

Mtume[saw] safari moja alipewa zawadi ya shuka ya hariri. Masahaba walishangaa kutokana na uzuri wake na ulainifu wake. Ndipo Mtume[saw] akasema ile leso aliyopewa Sa'ad bin Mu'az peponi ni nzuri na bora ziadi kuliko hii inayowashangaza.

Mtume[saw] akasema kutokana na kifo cha hadhrat Sa'ad bin Mu'az kiti cha enzi (cha Mwenyezi Mungu), kilitikisika, yaani kifo chake kilikuwa ni tukio kubwa la huzuni.

Hadhrat Mirza Bashir Ahmad sahib M.A[ra] anaeleza katika kitabu chake cha ***Siratun Nabii*** kuwa lile jeraha la hadhrat Sa'ad bin Mu'az[ra] alilolipata mkononi katika vita vya Ahzab halikuwa linapona. Kwa hiyo Mtume[saw] aliamuru kuwekwa hema msikitini ili matibabu yake yapatikane kwa urahisi na watu waweze kumtembelea ili kumwangalia. Akamweka mwanamke aliyekuwa mjuzi wa kutibu na kushona majeraha ili amshugulikie hadhrat Sa'ad bin Mu'az[ra] na kwa kawaida

Endelea uk 11

JARIDA LA KIINGEREZA





The Review of Religions

Jarida la *The Review of Religions* lilianzishwa na Masihi Aliyeahidiwa, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] mnamo mwaka 1902.

Lengo la kuanzishwa kwa jarida hili ni kuwasilisha mafundisho sahihi ya dini Tukufu ya Islam na kuangazia hekima, uhalisia, usawa na asili yake.

Jarida hili pia linajumuisha makala, maoni na mijadala juu ya falsafa za dini mbalimbali kwa kuzingatia heshima za Manabii na waanzilishi wa dini zote.

Dini Tukufu ya Islam inahimiza kutafuta elimu na *The Review of Religions* ni sehemu mahsusi kwa ajili ya kupata na kusambaza elimu.

Mratibu wa jarida la *The Review of Religions* nchini Tanzania, anawaomba wanajamaat wote wanaojua kusoma lugha ya Kiingereza kujiunga (Subscribe) ili kupata nakala ya jarida hilo kila mwezi.

Kwa maelezo zaidi ya namna ya kulipa na kujiunga wasiliana na maratibu kwa anuani zifuatazo:-

Sanduku la Posta: 376, Dar es salaam.
Namba ya Simu: **+255 713 386 435**
Barua pepe: **rnauja@gmail.com**







Gharama za Kujiunga ni Dola 30 ($30), na Dola 10 ($10) kwa wanafunzi kwa nakala 12

Kila atakayejiunga atatumiwa nakala 1 kila mwezi kwa mwaka mzima

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com